

SHULE YA SEKONDARI KALENGA – IRINGA

S.L.P 21, Ibangamoyo – Ulanda,

Iringa, Tanzania.

Simu: +255 767 551 371

+ 255 677 006 172

15/12/2020

Kumb Na. KSS/FI-2021/002

JINA LA MWANAFUNZI

S.L.P

.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KALENGA WILAYA YA IRINGA MKOA WA IRINGA MWAKA 2021

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **Kwanza (I)** katika shule hii mwaka **2021**. Shule ya Sekondari Kalenga ipo umbali wa Km 16.5 kutoka Iringa mjini barabara ya kuelekea Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Usafiri wa basi kutoka Iringa mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha **Stendi kuu ya Zamani**.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **06/01/2021** na unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **06.01.2020** bila kukosa.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

Sare ya shule ni **SURUALI 2 (Rangi nyeusi)** na **Mashati 2 meupe mikono mifupi** kwa wavulana na **Sketi 2 Nyeusi** na **Shati 2 Nyeupe mikono mifupi** kwa wasichana (kipande cha kitambaa kimeambatanishwa). Na pia **Sweta 1 rangi ya Kijani Jeshi / Kijani iliyokolea, soksi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana**.

a) Rangi ya Hijabu ifanane na sare za shule .

b) Sare za michezo kwa shule hii ni (tracksuit) nyeusi kwa wote

2.2 Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na, 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:-

a) Heshima kwa viongozi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la msingi.

- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii,
- f) Kutunza mwili usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Kutunza mali za umma

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

- a) wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevywa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau Bendera ya Taifa
- h) Kuwa mjamzito /kupata mimba
- i) Kutoa mimba
- j) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- l) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KALENGA SEKONDARI

.....
ANANIA N. KACHENJE
MKUU WA SHULE

**KALENGA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 21 IBAGAMOYO-ULANDA,
IRINGA
26/12/2020**

**MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL,**
.....
.....
.....

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Name of student

Please examine the above named student to his/her fitness as indicated below.

Please arrange for necessary treatment so that the certificate may be signed and brought to school by the student.

This certificate must be signed by a qualified medical officer of the Government Hospital.

Date Signature

MEDICAL CERTIFICATE.

I have examined the above named student with

Skin Abdomen

Eyes Stool

Ears Urine

Teeth..... H/B (haemoglobin)

Any other disabilities

1. I consider that he / she is
from infectious diseases, worms and is fit to come to school.
2. He / She is fit to come to school after having treatment of
3. She is not pregnant.
4. Other comments (if any)

.....
DATE

.....
MEDICAL OFFICER.